

HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI
MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI TAREHE 21/01/2022

KUMB.NA.MDC/TB/2021-2022 WALIOUDHURIA

A.WAJUMBE WALIOHUDHURIA

NA.	JINA	WADHIFA	CHEO
1.	Daniel Kamwela	Afisa Kilimo	Mwenyekiti
2.	Michael Kasenene	Afisa Ugavi	Katibu
3.	Eng.Abbas Kitalima	Mhandis Ujenzi	Mjumbe
4.	Kennedy Hincha	Afisa Nyuki	Mjumbe
5.	Raphael Shitindi	Afisa Usafi na Mazingira	Mjumbe
6.	Anna Shitindi	Afisa Elimu Sekondari	Mjumbe

KUMB.NA MDC/TB/2021-2022/01- KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa maudhurio yao, Akawataka kuwa makini, Kisha akafungua kikao mnamo saa 02:30 Asubuhi.

KUMB.NA MDC/TB/2021-2022/02- KUTHIBITISHA AGENDA

Katibu aliwasilisha agenda za kikao kama zinavyoonekana hapa chini;-

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha Agenda
3. Kupitia na kuthibitisha Muhtasari wa kikaocha bodi ya zabuni cha tarehe 15/10/2022
4. Kupitia taarifa tathimini jengo la dharura hospitali na nyumba ya watumishi iliyoko kijiji cha Mkandami (Three in one)
5. Manunuzi yaliyofanyika kwa njia ya round meeting robo ya pili
6. Pendekezo la kujenga jengo la kutolea huduma za dharula (EMD) na nyumba ya watumishi three in one zahanati ya Mkandami.
7. Mengineyo
8. Kufunga kikao

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kuthibitisha agenda za kikao zilizokuwa mbele yao.Wajumbe walikubali kuwa agenda hizo zijadiliwe.

KUMB.NA MDC/TB/2021-2022/03- KUPITIA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAOCHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE 15/10/2022

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kusoma na kupitia muhtasari wa kikao cha bodi ya zabuni cha tarehe15/10/2021., Masahihisho ya uandishi wa wajumbe yalifanyika na kisha ikapitishwa kuwa kumbukumbu kamili za vikao vya Bodi ya zabuni.

KUMB.NA MDC/TB/2021-2022/04- KUPITIA TAARIFA TATHIMINI JENGO LA DHARURA HOSPITALI NA NYUMBA YA WATUMISHI ILIYOKO KIJIKI CHA MKANDAMI (THREE IN ONE)

Katibu aliwasilisha taarifa ya thathimini ya jengo la dharura la hospitali na nyumba ya watumishi three in one.Aidha ufafanuzi ulitolewa kuwa kuna agizo la kutumia Force Account kujenga haya majengo.Wajumbe walipokea na kujadili kasha walishauri nyaraka ziwekwe zote kwani agenda hii ya kuoitia taarifa ya thathimini imeshafutwa kutokana na mabadiliko yaliyoletwa.

KUMB.NA MDC/TB/2021-2022/05- KUJADILI MANUNUZI YALIYOFANYIKA KWA NJIA YA ROUND MEETING ROBO YA PILI.

Katibu aliwasilisha taarifa ya manunuzi yaliyofanyika kwa utaratibu wa njia ya round meeting robo ya pili Tshs.459,334,555.04/=Wajumbe walipokea, kujadili na kupitisha kisha wakashauri PMU wajiridhishe viambatanisho muhimu kama EFD resiti, kuingiza kwenye store ledger n.k.Vimehakikiwa na kuambatanishwa kwa kumbukumbu.

KUMB.NA MDC/TB/2021-2022/06- PENDEKEZO LA KUJENGA JENGO LA KUTOLEA HUDUMA ZA DHARULA (EMD) NA NYUMBA YA WATUMISHI THREE IN ONE KATIKA ZAHANATI KIJJI CHA MKANDAMI.

Katibu aliwasilisha taarifa inayohitaka halmashauri kujenga jengo la kutolea huduma za dharura EMD na nyumba ya watumishi three in one katika zahanati ya Mkandami kwa kutumia force account , Wajumbe walipokea na kujadili kisha walipitisha ila walishauri iwe makini

AZIMIO

- Mhandisi aandae na alete BOQ tarehe 06 Januari asubuhi
- Fursa za mawe, mchanga na kokoto washirikishwe wananchi katika utekelezaji wa miradi hii na kuamasishwa

KUMB.NA MDC/TB/2021-2022/07 - MENGINEYO


Mengineyo kwa idhini ya mwenyekiti,


- Wajumbe walishauri kupata posho kwani hiki ni kikao halali cha bodi.
- Wajumbe walishauri kufanya mabadiliko ya kubadilisha mazingira ya kufanyia kikao

KUMB.NA MDC/TB/2021-2022/08 - KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa uvumilivu wao na ushiriki katika kikao na aliwatakia utekelezaji mwema wa yaliyojadiliwa kisha alikifunga kikao rasmi mnamo saa 04.16 Asubuhi

Muhtasari huu Umethibitishwa na


Daniel Kamwela
Mwenyekiti wa Kamati


Michael Kasenene
Katibu wa Bodi

Tarehe 21/01/2022